

SWALI: Mimi Nina MUNGU Wangu ambae Ni ALLAH
subhanallah...sasa kwanini nimkabidhi maisha Yesu wakati naye
alizaliwa Kama mimi?

JIBU: Mama yako alizaliwa kama wewe...lakini ilifika wakati
Mwenyezi Mungu aliyakabidhisha maisha yako kwake. Ili uwe
salama, ulindwe, uhifadhiwe, ulishwe na upendwe..na pamoja na
hayo ufundishwe kanuni za maisha ambazo peke yako bila wazazi
au mlezi usingeweza kujifunza.

Vivyo hivyo ulipaswa ukae chini ya sheria za wazazi wako ndipo
uweze kufanikiwa, endapo ungekuika sheria hizo basi maishani
usingefanikiwa....Na kama sio Mwenyezi Mungu kuyakabidhisha
maisha yako kwa wazazi wako ambao wamezaliwa kama wewe,
maisha yako yangukuwa magumu sana hapa duniani au hata
pengine usingezaliwa kabisa au kama ungezaliwa ungekufa.

Vivyo hivyo Yesu alizaliwa kama sisi tulivyozaliwa, (Ingawa
hakuzaliwa na dhambi ya asili kama sisi, kwasababu mimba yake
ilitungishwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu), na katika nyakati hizi
za uovu na mateso na dhiki za ulimwengu.

Kuna haja gani ya kumwamini Yesu aliyezaliwa kama sisi?

Mungu kwa huruma zake na kwa jinsi anavyotupenda akamtuma huyu Yesu Kristo, ili awe kama mzazi kwetu kwasababu sisi wenyewe hatutaweza kwa nguvu zetu na kwa akili zetu kujiongoza..Ndio maana hatuna budi wote tuyakabidhi maisha yetu kwake ili tuwe salama sasa na ahera.

Yohana 3:16 “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

17 Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye.

18 Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu”

Yesu anapoingia maishani mwetu, anatupa furaha, faraja, amani, upendo na tunapata ulinzi dhidi ya Adui shetani na mapepo yake yote, siku zote za maisha yetu na tumaini la uzima wa milele.

Kuna haja gani ya kumwamini Yesu aliyezaliwa kama sisi?

Bwana Yesu akubariki.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia masomo haya kwa njia ya email yako au Whatsapp tutumie ujumbe kwenye box la maoni chini au piga namba hii +255 789001312

Mada Nyinginezo:

KUOTA MAFURIKO, KUOTA MAJI MENGI, KUOTA MAWIMBI.

Ubatizo wa moto ni upi?

YULE JOKA WA ZAMANI.

Kuna haja gani ya kumwamini Yesu aliyezaliwa kama sisi?

KANUNI RAHISI YA KUFANIKIWA.

<https://wingulamashahidi.org/2018/07/04/5-swali-je-kuna-dhambi-kubwa-na-ndogo-na-kama-hakuna-je-mtu-aliyeya-na-aliyetukana-je-watapata-adhabu-sawa/>

JE NI DHAMBI KUWA NA MAHUSIANO KABLA YA NDOA?

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp